



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**MASAHIHISHO YA KATA ZITAKAZOFANYA UCHAGUZI MDOGO
WA MADIWANI TAREHE 22 JANUARI, 2017**

Kwa mujibu wa vifungu vya 13 (3) na 48 (2) vya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza jumla ya Kata **22** kuwa zitafanya Uchaguzi Mdogo kujaza nafasi wazi za Madiwani kwenye Halmashauri mbalimbali Tanzania Bara. Tangazo la Uchaguzi Mdogo wa Kata hizo lilitolewa katika Gazeti la Serikali la tarehe **02 Desemba, 2016** na katika Vyombo vya Habari mbalimbali vya kawaida.

Tume imepokea taarifa kuwa Kata ya **Mkoma** katika Halmashauri ya Wilaya ya **Rorya** na Kata ya **Mwamtani** katika Halmashauri ya Wilaya ya Itilima haziko wazi kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi.

Kata ya **Mkoma** Diwani wa Kata hiyo alishindwa Kesi yake katika Mahakama ya chini na sasa amekata Rufaa Mahakama ya juu (Mahakama Kuu) na hivyo, kufuatia hatua hiyo bado nafasi haiko wazi kwa kuwa Uamuzi unaweza kubadilika na kuendelea kuwa Diwani wa Kata hiyo.

Aidha, Diwani wa Kata ya **Mwamtani** alihukumiwa kifungo cha miezi sita (6) na tayari ametumikia kifungo hicho. Hivyo, kwa mujibu wa Sheria, Diwani huyo bado ana sifa za kuendelea kuwa Diwani wa Kata hiyo. Tume imefuatilia na imejiridhisha kuwa Kata hizo ni kweli haziko

wazi kwa mujibu wa Sheria na imetoa Uamuzi wa kuziondoa Kata za **Mkoma** na **Mwamtani** katika orodha ya Kata zilizotangazwa na Tume kufanya Uteuzi wa Wagombea tarehe **22 Desemba, 2016** na baadaye kufanya Uchaguzi tarehe **22 Januari, 2017** kujaza nafasi wazi.

Kwa msingi huo, Tume inapenda kufahamisha Vyama vya Siasa, Wadau wa Uchaguzi na Wananchi kwa ujumla kuwa Kata za **Mkoma** katika Halmashauri ya **Rorya** na **Mwamtani** katika Halmashauri ya **Itilima** hazitafanya Uchaguzi Mdogo kama zilivyotangazwa hapo awali. Kata zitakazo husika na Uchaguzi Mdogo ni 20 ambazo ni:-

NA.	MKOA	NA.	HALMASHAURI	NA.	KATA
1.	Dodoma	1.	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.	1	Ng'hambi
		2.	Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.	2	Ihumwa
2.	Morogoro	3.	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.	3	Kiwanja cha Ndege
3.	Iringa	4.	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.	4	Igombavanu
			Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.	5	Ikweha
4.	Arusha	5.	Halmashauri ya Wilaya ya Meru.	6	Ngarenanyuki
5.	Dar Es Salaam	6.	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.	7	Kijichi
6.	Singida	7.	Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.	8	Kinampundu
7.	Shinyanga	8.	Halmashauri ya Mji wa Kahama.	9	Isagehe
8.	Katavi	9.	Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe.	10	Kasansa
9.	Mwanza	10.	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.	11	Malya
		11.	Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.	12	Kahumulo

NA.	MKOA	NA.	HALMASHAURI	NA.	KATA
10.	Ruvuma	12.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.	13	Maguu
		13.	Halmashauri ya Manispaa ya Songea	14	Tanga
11.	Kagera	14.	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba.	15	Kimwani
12.	Geita	15.	Halmashauri ya Wilaya ya Geita.	16	Nkome
13.	Kilimanjaro	16.	Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.	17	Lembeni
14.	Manyara	17.	Halmashauri ya Wilaya ya Babati.	18	Duru
15.	Pwani	18.	Halmashauri ya Mji Kibaha.	19	Misugusugu
16.	Arusha	19.	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.	20	Mateves

Imetolewa na:-

Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI